

## **IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI.**

### **TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA ROBO YA TATU 2018.**

#### **1. UTANGULIZI**

Halmashauri ya wilaya ya Ngara ina jumla ya shule za sekondari 29, kati ya hizo 23 ni za serikali na 6 ni za binafsi. Kuna shule 4 zinazotoa elimu ya juu ya sekondari, 3 za serikali na 1 ya binafsi. Jumla ya wanafunzi katika wilaya ya Ngara ni **12053** kati ya hao wanafunzi wa shule za serikali ni was **5203** wav **5059** jml **10262** Wanafunzi wa shule za binafsi ni 1791 was **1008** wav **783** jumla **1791**.

#### **2. UFUATILIAJI WA TAALUMA SHULENI**

Katika kipindi cha kuanzia Julai mpaka Septemba idara ilifanikiwa kutembelea shule kwa ajili ya ufuatiliaji wa maendeleo ya taaluma, utawala, miundombinu na utekelezaji wa masuala mtambuka. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kupitia nyaraka za kufundishia na kujifunzia kama vile maandalio ya masomo, maazimio ya kazi, shajala na nyingine, ukarabati wa samani na upandaji miti. Shule zilizotembelewa ni Kanazi, Shunga, Ngara, Muyenzi, Ntobeye, Kabanga, Nyabisindu, Ndomba, Kibimba, Keza, Nyakisasa na Murusagamba.

#### **3. KUAJIRIWA WALIMU WA SAYANSI**

Kwa kipindi hiki Idara ya elimu sekondari ilipokea walimu 4 wa ajira mpya kwa masomo ya sayansi na kufikia jumla ya walimu wa sayansi waliopo 76 na kupunguza mahitaji na kufikia walimu 79.

#### **4. MITIHANI YA KIDATO CHA PILI 2017**

Shule 28 zilifanya mtihani huu wa Taifa wa kidato cha pili 2017 na jumla ya watahiniwa **2382** walifanya mtihani huo. Aidha kati ya hao 2173 walipata daraja I-IV sawa na asilimia 92 na watahiniwa 209 sawa na asilimia 8 walifeli na kurudia kidato ha pili. Mwaka 2018. *Jedwali namba 1 limeambatanishwa.*

#### **5. MITIHANI KIDATO CHA NNE 2017**

Shule 28 zilifanya mtihani huu wa Taifa wa kidato cha nne Novemba 2017 na jumla ya watahiniwa **1511** walifanya mtihani huo. Aidha kati ya hao daraja I-40, II-174, III-297, IV-688 na daraja 0-312. Waliopata daraja I-V ni 1199 sawa na asilimia 79.3 na daraja 0 ni 312 sawa na asilimia 20.7. *Jedwali namba 2. Limeambatanishwa.*

#### **6. UCHAGUZI WA KIDATO CHA KWANZA 2018**

Uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha kwanza 2018 kwa ujumla wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kidato cha kwanza Januari 2018 ni wavulana 1838 na wasichana 1988 jumla yao ni wanafunzi 3826 sawa na 100% ya waliofaulu.

Aidha, wanafunzi 3813 wavulana 1830 na wasichana 1983 watajiunga na shule za sekondari 23 za Halmashauri ya Ngara na wanafunzi 13 wavulana 8 na wasichana 5 watajiunga na shule za vipaji. *Jedwali namba 3. Limeambatanishwa kwa kila shule.*

## 7. MAPOKEZI YA FEDHA ZA ELIMU BILA MALIPO.

Idara ya elimu sekondari kupitia shule za sekondari 23 imekuwa ikipokea fedha za elimu bila malipo kuanzia disemba 2015 kwa kuzingatia idadi ya wanafunzi kwa kila shule kwa mwaka.

Aidha kwa kipindi cha Januari-Machi 2018 shule za sekondari zimepokea kiasi cha fedha Tshs. zimepokelewa ikiwa ni fedha za fidia ya ada kwa shule za kutwa Tshs. **25,425,297.00**, chakula kwa wanafunzi wa bweni tshs **115,528,416.00** fedha ya uendeshaji Tshs. **18,685,476.00** na posho ya madaraka kwa wakuu wa shule Tsh **11,500,000.00**

## 8. MAPOKEZI YA FEDHA ZA (EP4R)

Kwa kutumia vigezo vya program Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs 506,806,136.48** katika idara ya Elimu Msingi na Sekondari ni kama ifuatavyo:

NA	SHUGHULI	ASILI MIA	KIASI CHA FEDHA	IDARA	
				MSINGI	SEKONDARI
1	TAKWIMU (UKUSANYAJI, USIMAMIZI WA ELIMU, UFUATILIAJI NA TATHIMINI)	10	50,680,713.65	35,476,499.55	15,204,214.09
2	UPANGAJI WA IKAMA ELIMU MSINGI	20	101,361,427.30	101,361,427.30	0
3	UJENZI WA MADARASA MAPYA	40	202,722,854.59	142,722,854.59	60,000,000.00
4	UKAMILISHAJI WA MAABARA	30	152,042,140.94	0	152,042,140.94
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>100</b>	<b>506,807,136.48</b>	<b>279,560,781.45</b>	<b>227,246,355.03</b>

## 9. MIUNDOMBINU

Pamoja na changamoto mbalimbali za upatikanaji wa fedha Serikali na wadau mbalimbali wameendelea kuchangia na kuboresha miundombinu kama ifuatavyo;

NA.	AINA YA MIUNDOMBINU	YALIYOMO	ASILIMIA
1	Vyumba vya Madarasa	264	100
2	Nyumba za Walimu	91	18
3	Matundu ya Vyoo	302	66
4	Ofisi za Walimu	13	57
5	Meza	8736	85
6	Viti	8900	86
7	Maabara	22	32

## **10. MAFANIKIO**

- Serikali imekuwa ikipeleka Fedha ya elimu bila malipo kwa wakati kwenye shule zetu zote 23 na kufanikisha uendeshaji wa shule.
- Kuongezeka kwa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kwa mwaka 2018 kutoka 3288 hadi 3826
- Serikali kuajiri walimu wa masomo ya sayansi na mtaalamu wa maabara
- Kuongezeka kwa mabweni katika shule za Murusagamba 2 na muyenzi 1
- Kuongezeka kwa matundu ya vyoo shule ya sekondari Murusagamba 10 na Nyamiaga 6
- Kuongezeka kwa madarasa shule za Murusagamba 4 na Nyamiaga 1.
- Kuongezeka kwa maabara kutoka 17 hadi 22.
- Kufanikisha uendeshaji wa mitihani ya ndani 3na ya kitaifa.

## **11. CHANGAMOTO.**

- Upungufu wa walimu wa sayansi na hisabati na wataalamu wa maabara katika shule zetu
- Kutokamilika kwa ujenzi wa maabara, katika maabara 69 ni 22 tu ndio zilizokamilika.
- Kuwepo kwa upungufu wa madawati baadaya kuongezeka kwa wanaojiunga kidato cha kwanza.
- Upungufu wa vyoo kwa vyoo, madarasa kwa baadhi ya shule baadaya kuongezeka kwa wanafunzi kidato cha kwanza.
- Kutokuwepo kwa majengo ya utawala

## **12. UFUMBUZI.**

- Kuwashirikisha wananchi katika kuendelea kuchangia miradi ya maendeleo.
- Kuwashirikisha wadau mbalimbali wa elimu kuendelea kuchangia elimu kwa ujumla
- Kuendelea kuikumbusha Serikali kutuma fedha za miradi kama zilivyopangwa kwenye bajeti.
- Kuendelea kuwahimiza walimu kutimiza wajibu wao katika ufundishaji.

### 3.0. IDARA YA ELIMU MSINGI:

Katika kipindi cha **Januari – Machi, 2018** Idara ya Elimu ya Msingi imetekeleza shughuli zifuatazo:

#### A. SHUGHULI ZA KAWAIDA:

S/NA	SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAFANIKIO / CHANGAMOTO
1.	Usajili wa watahiniwa kwenye mitihani ya kitaifa kupitia mfumo wa PREM	<ul style="list-style-type: none"> <li>Watahiniwa <b>5,098</b> (Wav <b>2.391</b> na Was <b>2,704</b>) wamesajiliwa kufanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi mwezi Septemba, 2018</li> <li>Watahiniwa <b>7,602</b> (Wav <b>3.760</b> na Was <b>3.842</b>) wamesajiliwa kwa ajili ya upimaji wa darasa la Nne mwezi Novemba, 2018.</li> <li>Wanatahiniwa <b>5</b> (Wav <b>3</b> Na Was <b>2</b>) wamesajiliwa kwa ajili ya kufanya mtihani wa Ufundi Stadi mwezi Novemba, 2018</li> </ul>	<p>Utoro wa baadhi ya wanafunzi katika shule.</p> <p><b>Utatuji:</b> Kamati za shule zimeelekezwa kusimamia wanafunzi hao kila siku ili waweze kufanya mitihani yao ya mwisho wa mwaka.</p>
2.	Kusimamia zoezi la uandikishaji wa wanafunzi wa Darasa la I na Awali kuanza mazomo mwaka 2018	<p>Wanafunzi <b>11,483</b> (Wav <b>5,847</b> na Was <b>5636</b>) walitarajiwa kuandikishwa darasa la I. Hadi sasa wanafunzi <b>14,071</b> (Wav <b>6,977</b> na Was <b>7094</b>) sawa na asilimia <b>123</b> wameandikishwa.</p> <p>Aidha wanafunzi <b>14,692</b> (Wav <b>7,507</b> na Was <b>7,185</b>) walitarajiwa kuandikishwa Darasa la Awali. Hadi sasa wanafunzi <b>12,875</b> (Wav <b>6,505</b> na Was <b>6,370</b>) sawa na asilimia <b>88</b> wameandikishwa.</p>	<p>Ongezeko hilo la Uandikishaji limeleta changamoto ya upungufu wa miundo mbinu shule mfano vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na madawati.</p> <p>Hadi sasa kuna upungufu wa madarasa <b>821</b> matundu ya vyoo <b>1,859</b> na madawati <b>902</b>.</p> <p><b>Utatuji:</b> Wananchi wameendelea kuhamasishwa kuongeza miundo mbinu kwenye shule mfano hadi sasa vyumba vya madarasa <b>20</b> vinaendelea kujengwa.</p>
3.	Kuendesha mikutano ya Maafisa Elimu Kata na Walimu Wakuu.	Katika jitihada za kuinua taaluma mwaka 2018 Idara imefanya vikao vya Walimu Wakuu na Maafisa Elimu Kata kati ya tarehe 4 na 5.01.2018	Walimu Wakuu na Maafisa Elimu Kata wamekumbushwa na kusesitizwa juu ya jukumu lao la kusimamia na kushirikisha jamii katika kuongeza miundo mbinu shuleni.
4.	Kufanya mikutano na walimu wote.	Idara imefanya vikao vya walimu wote tarehe 05.03.2018 - 04.03.2018 kwa ajili ya kuhimiza suala la taaluma.	Walimu wote wamekubaliana kuongeza ufaulu katika mitihani ya kitaifa kutyoka asilimia <b>80</b> - (2017) hadi <b>90</b> (2018) Darasa la VII na

S/NA	SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAFANIKIO / CHANGAMOTO
			kutoka asilimia <b>98</b> - (2017) hadi <b>99</b> (2018) katika upimaji wa Darasa la Nne.
5.	Mapokezi ya walimu kwenye idara.	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Idara imepokea walimu wanne (4) walioajiliwa Januari, 2018. Walimu hao walipangiwa shule zao na OR – TAMISEMI ambazo ni Kanyinya, Kasange, Kagali na Kabulanzwiri.</li> <li>• Idara imepokea walimu <b>22</b> waliohamishiwa toka Idara ya Elimu ya Sekondari. Walimu hao wamepangiwa shule zilizopo kwenye maeneo ya shule walikotoka Kama maelekezo yalivyotolewa.</li> </ul>	Pamoja na mahitaji makubwa ya walimu 22 kupokelewa kwa walimu kumepunguza kwa kiasi kidogo upungufu wa walimu kwenye shule walizopangiwa.
6.	Mapokezi ya fedha za motisha (EP4R)	<p>Halmashauri imepokea <b>Shs.506, 807,136.48</b> baada ya kukidhi vigezo kwenye mwaka wa fedha 2016/17. Fedha hizo zitatumika katika maeneo manne (4)</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Ukusanyaji wa Takwimu, usimamizi wa Elimu, ufuatiliaji na tathmini Shs.50, 680,713.65.</li> <li>• Upangaji wa Walimu <b>Shs.101, 361,427.30.</b></li> <li>• Ujenzi wa madarasa mapya <b>Shs. 202,722,854/=</b></li> <li>• Ukamilishaji wa maabara <b>Shs. 152,042,140.94.</b></li> </ul>	<p>Upatikanaji wa fedha hizi utasaidia kupunguza kwa kiasi fulani changamoto zinazokabili idara za Elimu.</p> <p>Lengo kutumia fedha hizo kadri ya maelekezo yalivyo ili Halmashauri iweze kupata zaidi ya Shs.700, 000,000/= mwaka 2019.</p>
7.	Ufuatiliaji wa miradi itakayopata fedha za motisha (EP4R).	<p>Ili kubaini ni miradi ambayo imechangiwa zaidi na nguvu za wananchi ili iweze kupatiwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji.</p> <p><b>Lengo:</b> Kuwa na miradi michache itakayokamilishwa kikamilifu.</p>	Miradi iliyoanzishwa na wananchi ni mingi kulinganishwa na kiasi cha fedha kilichopo.

**B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO – ROBO YA TATU  
JANUARI – MACHI - 2017/2018.**

<b>NA</b>	<b>AINA YA MRADI</b>	<b>KIASI TENGWA</b>	<b>KIASI TOLEWA</b>	<b>MAELEZO</b>
	Kukamilisha ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za msingi ya Bugarama, Nyakafandi, Mukididili, Murukagati, Nyamahwa, Mukibogoye, Kumutana, Mukirehe, Buhororo, Kagali, kasulo, Ntukamazina, Ntobeye na Ngundusi	200,000,000	0.00	Ujenzi bado kuanza kwa sababu serikali haijaleta ruzuku
	Kukamilisha ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa shule za msingi Bukiriro, Kumubuga and Rwimbogo.	36,000,000	0.00	Ujenzi bado kuanza kwa sababu serikali haijaleta ruzuku
	Ujenzi wa vyoo katika shule za Shanga, Murukagati, Murusagamba, Mukarehe, Mubinyange, Murugalagala, Muyenzi, Njiapanda, Nyarusange, Mumuhamba, Kashinga, Ngoma, Kititiza, Mwivuza B na Ruganzo B	96,000,000.00	0.00	Ujenzi bado kuanza kwa sababu serikali haijaleta ruzuku

**Viambatanisho:**

***Kiamb. Na. 1:** Orodha ya walimu waliohamishiwa Idara ya Elimu ya Msingi toka Idara ya Elimu ya Sekondari.*

***Kiamb. Na 2:** Taarifa ya Mapokezi ya fedha za motisha (EP4R) mwaka 2018.*

***Kiamb. Na. 3:** Taarifa ya mapokezi ya fedha za Elimu bila malipo kwa kipindi cha miezi 8 (Julai, 2017 hadi Februari, 2018) kwa shule za msingi.*